

**1. Who is Jesus?**

- a. God the Son – Jesus’ divinity.
- b. Jesus of Nazareth – Jesus’ humanity.
- c. Christ – Jesus’ office.

**2. Why did Jesus come?**

- a. “Savior”
- b. “Lord”

**3. So what?**

- a. Believe.
- b. Worship.
- c. Live true lives.

## Luka 2:1-20

**1** Siku zile amri ilitoka kwa Kaisari Augusto ya kwamba iandikwe orodha ya majina ya watu wote wa ulimwengu.**2** Orodha hii ndiyo ya kwanza iliyoandikwa hapo Kirenio alipokuwa liwali wa Shamu.

**3** Watu wote wakaenda kuandikwa, kila mtu mjini kwao.**4** Yusufu naye aliondoka Galilaya, toka mji wa Nazareti, akapanda kwenda Uyahudi mpaka mji wa Daudi, uitwao Bethlehemu, kwa kuwa yeye ni wa mbari na jamaa ya Daudi;**5** ili aandikwe pamoja na Mariamu mkewe, ambaye amemposa, naye ana mimba.**6** Ikawa, katika kukaa huko, siku zake za kuzaa zikatimia,**7** akamzaa mwanawe, kifungua mimba, akamvika nguo za kitoto, akamlaza katika hori ya kulia ng'ombe, kwa sababu hawakupata nafasi katika nyumba ya wageni.**8** Na katika nchi ile ile walikuwako wachungaji wakikaa makondeni na kulinda kundi lao kwa zamu usiku.**9** Malaika wa Bwana akawatokea ghafula, utukufu wa Bwana ukawang'aria pande zote, wakaingiwa na hofu kuu.**10** Malaika akawaambia, Msiogope; kwa kuwa mimi ninawaletea habari njema ya furaha kuu itakayokuwa kwa watu wote;**11** maana leo katika mji wa Daudi amezaliwa, kwa ajili yenu, Mwokozi, ndiye Kristo Bwana.**12** Na hii ndiyo ishara kwenu; mtamkuta mtoto mchanga amevikwa nguo za kitoto, amelala katika hori ya kulia ng'ombe.**13** Mara walikuwapo pamoja na huyo malaika, wingi wa jeshi la mbinguni, wakimsifu Mungu, na kusema,**14** Atukuzwe Mungu juu mbinguni, Na duniani iwe amani kwa watu aliowaridhia.**15** Ikawa, malaika hao walipoondoka kwenda zao mbinguni, wale wachungaji waliambiana, Haya, na twendeni mpaka Bethlehemu, tukalione hilo lililofanyika, alilotujulisha Bwana.**16** Wakaenda kwa haraka wakamkuta Mariamu na Yusufu, na yule mtoto mchanga amelala horini.**17** Walipomwona wakatoa habari waliyoambiwa juu ya huyo mtoto.**18** Wote waliosikia wakastaajabu kwa hayo waliyoambiwa na wachungaji.**19** Lakini Mariamu akayaweka maneno hayo yote, akiyafikiri moyoni mwake.**20** Wale wachungaji wakarudi, huku wanamtukuza Mungu na kumsifu kwa mambo yote waliosikia na kuyaona, kama walivyoambiwa.